BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 26 Mei, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Afya:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

195. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna vituo vingapi na wapi ambapo Serikali imevijenga kwa ajili ya kuwaweka wajasiriamali kufanya biashara zao katika mazingira bora na ya kuridhisha.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

117. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Wajasiramali kinamama wauza uji ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe wanafanyakazi kubwa sana ya kuisaidia jamii ya kipato cha chini kuwajengea lishe bora katika maisha yao.

    Ni kwa kiasi gani Serikali itawaona kwa jicho la huruma na kuwapatia mikopo nafuu na mitaji ili kuendeleza kampeni ya lishe bora kwa jamii.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

178. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Ni yepi matarajio ya uwekezaji katika eneo linalomilikiwa na ZSSF liliopo Tunguu ambalo kwa muda mrefu limekuwepo bila ya matumizi yoyote.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

292. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Msongamano mkubwa wa gari unasababishwa na kukosekana kwa barabara za kutosha za michepuko, uingiaji na utokaji wa gari kubwa bandarini na gari kubwa za usafirishaji, gari za mchanga kutumia barabara hizo hizo ambazo ni nyembamba na zinatumiwa na watu wote (hasa njia ya Bububu).

    Ni lipi suluhisho la tatizo hili, ukizingatia pia linaongeza ajali za barabarani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

182. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni mambo gani ya msingi ya kujivunia katika awamu hii ya Dkt. Mwinyi kupitia sekta ya mageuzi ya tasnia ya habari kwa ujumla wake.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

67. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Migogoro ya ardhi ni kadhia kubwa kwa baadhi ya wananchi wetu.

Je, Wizara yako inatumia njia zipi za utatuzi wa migogoro hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

224. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tathmini ya uwekezaji katika vyuo vya umahiri wa ujuzi wa kada za kati ipo vipi kwa muktadha wa mabadiliko ya kimtaala.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

235. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kumekuwa na urejeshaji mdogo wa mikopo ya boti za uvuvi na mwani zipatazo 1,027 walizokopeshwa wananchi.

(a) Je, Wizara yako inalitambua vipi suala hili.

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani za kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inarudishwa kwa wakati kama ilivyoelezwa katika mikataba waliyopewa wananchi hao.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

148. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni nyumba ngapi na zipi ndani ya eneo la Mji Mkongwe wa kihistoria wa Zanzibar zimefanyiwa ukarabati kwa miaka ya hivi karibuni.

(b) Ni yepi matarajio ya Serikali katika kuuendeleza mji huo kuwa na sura ile ile ya uwepo wa watu wa mataifa na makabila mbali mbali.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

159. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kihistoria Zanzibar imejijengea umaarufu mkubwa kuwa ni kisiwa cha viungo (Spice Island) kutokana na kushamiri kwa biashara hii hususani katika karne ya 19.

Kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa uzalishaji wa miti ya viungo hivi karibuni, Serikali inafanya jitihada zipi kuirejesha imani ya ukweli kwamba Zanzibar ni visiwa vya viungo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2025/2026.

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**26 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**